



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA.



Kumb: Na. SHY/MC/S. 20/32 VOL.II/28

Tarehe: 28. 08. 2023.

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kupitia barua ya Katibu Mkuu Utumishi yenye Kumb.Na. FA.170/376/01"B"/139 ya tarehe 11/07/2023 alipewa kibali cha ajira mbadala, hivyo Mkurugenzi wa Manispaa anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa za kuomba nafasi ya **Msaidizi wa Kumbukumbu II** kama ifuatavyo:

MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II NAFASI MBILI (2)

SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na Cheti cha kuhitimu na kufaulu kidato cha Nne (IV) au sita.
- ii. Awe na stahada au NTA level 6 katika mojawapo ya fani zifuatazo; utunzaji wa kumbukumbu, urasimu ramani (Cartography) au Geoinformatics), Sheria au Kumbukumbu za Afya kutoka katoka vyuo vinavyotambulika na Serikali.
- iii. Awe na ujuzi wa kompyuta.
- iv. Awe raia wa Tanzania mwadilifu na mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45

MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kuorodhesha barua zinazolingia masjala kwenye rejista (incoming correspondence register)
- ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi kwenye rejista (outgoing correspondence register)
- iii. Kusambaza majalada kwa watendaji (action officers)
- iv. Kupokea majalada yanayotoka kwa watendaji
- v. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya taasisi (file tracking)
- vi. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga nyaraka za taasisi katika majalada kulingana na somo husika (classification indexing)

- vii. Kupanga na kudhibiti nyaraka katika vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu (repositories).
- viii. Kuwasimamia wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo.
- ix. Kurudisha majalada yaliyosomwa kwenye ghala la kuhifadhia nyaraka.

MASHARTI YA KAZI

Ni ajira ya kudumu (TGS, C)

MASHARTI YA JUMLA

- i. Awe ni raia wa Tanzania
- ii. Mwombaji aliyewahi kupatikana na kosa la jinai hatafikiriwa
- iii. Barua zote zitumwe kupitia Posta. Barua zitakazoletwa kwa mkono hazitapokelewa
- iv. Aidha barua ya mwombaji ioneshe anwani anayotumia kwa sasa pamoja na namba za simu ikiambatishwa na;
 - (a) Maelezo binafsi ya mwombaji (CV)
 - (b) Nakala ya vyeti vya elimu na Taaluma
 - (c) Nakala ya cheti cha kuzaliwa
 - (d) Nakala ya kitambulisho cha Nida au Namba
- iv. Weka picha mbili (2) za passport size za hivi karibuni
- v. Watakaoteuliwa kuhudhuria usaili (interview) watafahamishwa kupitia anwani na namba za simu walizotumia kwenye barua zao za maombi ya kazi
- vi. Transcripts, Testimonials and Provisional Results havitakubalika
- vii. Nakala zote za vyeti vya Shule, Chuo na Cheti cha kuzaliwa zithibitishwe na Mwanasheia au Wakili yeyote aliyesajiwa na kuthibitishwa.
- viii. Waombaji wote wawe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- (x). Mwombaji aombe kwa kuzingatia masharti ya **TANGAZO LA KAZI**.
- (XI) Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.

JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote ziandikwe kwa mkono wa mwombaji na kutumwa kwa;

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Manispaa,
S.L.P. 28,
SHINYANGA.

Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe **11/09/2023** Siku ya jumatatu saa 9:30
alasiri.

Tangazo hili limetolewa na:


Mwl. Alexius R. Kagunze

MKURUGENZI WA MANISPAA

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
SHINYANGA